كنوز الصلاة - سواحيلي

# HAZINA ZA SWALA



جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

288

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# HAZINA ZA SWALA

## كنوز الصلاة - سواحيلي


جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي

هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# كنوز الصلاة - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**


**ⓗجمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ**

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
كنوز الصلاة / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد
وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ
٥٢ ص ؛ ..سم

ردمك: ٢-٠٠-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الصلاة أ.العنوان

ديوي ٢٥٢,٢ ١٤٤٤/٥٨٠٨

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٠٨**
**ردمك: ٢-٠٠-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

# Kutawadha

Udhu una fadhila nyingi na kubwa miongoni mwa hizo:

* **Kupata Mapenzi ya Allah**:
Kama Allah Mtukufu Anavyosema: *"Hakika Allah Anawapenda wenye kutubu, na Anawapenda wenye kujitwaharisha." [Al - Baqarah : 222]*.

* **Kufutiwa makosa na kupandishwa daraja.**
Imepokewa na Abu Hurairah – Allah Amridhie - ya kwamba Mtume - Rehema za Allah na Amani zimshukie - amesema: *"Mja Muislamu au Muumini anapotawadha na kuosha uso wake, kila dhambi aliyoitazama kwa macho yake, hutoka kwa maji aliyooshea uso wake, au kwa tone la mwisho la maji. Kisha akiosha mikono yake, hutoka mikononi mwake kila dhambi aliyoifanya kwa mikono yake, hutoka kwa maji aliyooshea mikono yake, au kwa tone la mwisho la maji. Kisha anapoosha miguu yake hutoka kila dhambi ambayo Miguu yake ilitoka kwenda kuitenda, hutoka na maji aliyooshea*

*miguu yake, au kwa tone la mwisho la maji - mpaka atoke akiwa ametakasika na madhambi."* [Imepokewa na Muslim: 577].

* Na anapokea pia Abu Hurairah - Allah Amridhie - amesema: ya kwamba Mtume - Rehema za Allah na Amani zimshukie - amesema: *"Je! Nisikuambieni kwa njia gani Allah Hufuta madhambi na Hunyanyua daraja?"* Wakasema: "Tuambie, Ewe Mtume wa Allah." Akasema: *"Kutawadha wakati wa ugumu, na hatua nyingi za kwenda Misikitini, na kungojea Swala baada ya Swala, hiyo ndiyo Riba-at, (kujizuia kuliko bora zaidi)..."*. [ameipokea Muslim: 587]

***Na wakati wa ugumu: Ni mfano wa baridi kali au joto au ugonjwa, au mfano wa hayo.***

* Na kutoka kwa Uthman Ibn Affan amesema: Mtume – Rehema za Allah na Amani zimshukie - amesema, *"Mwenye kutawadha vizuri basi dhambi zake zitatoka mwilini mwake mpaka zitatoka chini ya kucha zake."* [Ameipokea Muslim:578]

## Dhikr (Uradi) baada ya Kutawadha

Dhikri baada ya kutawadha zina fadhila kubwa ambayo hutakiwi kuipoteza ewe ndugu yangu uliyebarikiwa. Basi pata bishara hii nzuri kutoka kwa mkweli mwenye kukubaliwa maneno yake - Rehema na za Allah na Amani zimshukie:-

* Kutoka kwa 'Umar Ibn al-Khattab - Allah Amridhie - amesema: Mtume – Rehema za Allah na Amani zimshukie – amesema, *"Hakuna miongoni mwenu anayetawadha akatawadha kwa ukamilifu kisha akasema: 'Nashuhudia ya kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, na ya kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake, isipokuwa hufunguliwa milango minane ya Peponi, aingie wowote aukatao."* [Imepokewa na Muslim: 553].

## Mswaki

* Kutoka kwa Abu Hurayrah – Allah Amridhie - amesema: Mtume – Rehema na Amani za Allah zimfikie - amesema, *"Lau nisingehofia kupata ugumu umma wangu, ningeliwaamrisha kutumia mswaki katika kila Swala."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 887, 252].

* Na Kutoka kwa - mama wa waumini - Aisha, - Allah Amuwie Radhi - amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah zimfikie amesema:- *"Mswaki ni kisafisha kinywa na kinamridhisha Mola mlezi."* [Imepokewa na An-Nasa'iy: 5].

**Kuwahi Mapema Kwenda Kuswali**

Ubora wa kufika mapema katika Swala na malipo yake ulibainishwa na Mtume wetu Mtukufu - Rehema na Amani za Allah zimfikie - katika hadithi nyingi, zikiwemo:

*Kutoka kwa Abu Hurayrah – Allah Amridhie- amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah zimfikie amesema:- *"Lau watu wangejua (thawabu) zilizomo katika wito (Adhana) na safu ya kwanza, kisha wasipate njia ya kulifikia hilo ila kwa kupiga kura, wangepiga kura kwa ajili ya hilo, na wakijua kilichomo katika kuwahi mapema (Swala) wangeshindana kuiendea hiyo Swala..."*. [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 615, 981]

*Kutoka kwa Abu Said al-Khudri – Allah Amridhie - kwamba Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - Aliona baadhi ya

Masahaba zake wanakawia (wanachelewa kujiunga katika Swala) akawaambia: *"Sogeeni mbele na nifuateni mimi, na wawafuateni ninyi walio baada yenu. Watu hawatakawia (kujiunga kwenye Swala) mpaka Allah atawachelewesha (kuwapa daraja ya juu)*." [Imepokewa na Muslim: 982]

* Na kufika mapema kwenye Swala ni dalili ya kushikamana kwa moyo na msikiti. Imekuja katika hadithi ya wale watu saba ambao Allah atawaweka chini ya kivuli chake, siku ambayo hakuna kivuli ila chake, kwamba miongoni mwao: *"...na mtu ambaye moyo wake umetundikwa Misikitini..."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 1423, 2380]

## Kuyarejea Maneno ya Adhana

*Kutoka kwa Abdullah bin Amri - Allah Awawiye radhi - kuwa yeye alimsikia Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - akisema: *"Mkisikia muadhini, basi semeni sawa na anayoyasema, na kisha mniswalie mimi, hakika atakaeniswalia mara moja, Allah Atamrehemu yeye mara kumi..."* [Imepokewa na Muslim: 849].

*Kutoka kwa ‘Umar bin al-Khattab – Allah Amridhie - amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *“Akisema Muadhini: Mungu ni Mkubwa zaidi, Mungu ni Mkubwa zaidi, na mmoja wenu aseme: “Mungu ni Mkubwa zaidi, Mungu ni Mkubwa zaidi.” Kisha akisema: “Nashuhudia kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah.” Naye aseme: Nashuhudia kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah.” Kisha akisema: ‘Njooni kwenye Swala.’ Naye aseme: ‘Hakuna nguvu wala uwezo ila wa Allah.” Kisha akisema: “Njooni kwenye ufaulu.” Asema: “Hakuna nguvu wala uwezo ila wa Allah.” Kisha akisema: “Mungu ni Mkubwa zaidi, Mungu ni Mkubwa zaidi.” Akisema: ‘Mungu ni Mkubwa zaidi, Mungu ni Mkubwa zaidi.’ Kisha akisema: ‘Hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah.’ Aseme: ‘Hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, (akisema hayo) moyoni mwake, ataingia Peponi.”* [Imepokewa na Muslim: 385].

## Kuleta Uradi (Dhikri) baada ya Adhana

Miongoni mwa hazina za Ibada hii kubwa:

* **Kusamehewa madhambi:**

Kwa hadithi iliyopokelewa na Saad bin Abii Waqqas - Allah Amridhie - kutoka kwa Mtume - Rehema za Allah na Amani zimshukie - kwamba amesema: *"Mwenye kusema asikiapo muadhini: 'Nashuhudia ya kwamba hapana mola ila Allah Pekee ambaye hana mshirika, na kwamba Muhammad ni mja na Mtume wake, mimi nimeridhika na Allah kuwa ni Mola Mlezi, na Muhammad kuwa ni Mtume, na Uislamu kuwa ni Dini, atasamehewa madhambi yake."* [Imepokewa na Muslim: 851].

* **Uombezi wa Mtume –Rehema za Allah zimshukie-:**

Kutoka kwa Jabir bin Abdillah - Allah Amuwiye radhi - kwamba Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mwenye kusema anaposikia mwito (Adhana): Ewe Mola Mlezi wa wito huu mkamilifu na swala iliyothibiti, mpe Muhammad daraja ya juu katika pepo, na fadhila, na umnyanyue kwenye nafasi iliyotukuka uliyomuahidi - isipokuwa uombezi*

*wangu utatolewa kwake Siku ya Kiyama*" [Imepokewa na Al-Bukhari: 614].

## Kutembea Kwenda Kuswali

Kutembea wakati wa kwenda kwenye Swala ni kupanda daraja na kafara ya maovu. Na mwenye kwenda msikitini asubuhi na jioni, ameandaliwa nyumba ya Peponi kila aendapo au arudipo. Bali hakika Mtume – Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - anatupa habari njema zaidi ya hizo:

* Kutoka kwa Abu Hurayrah - Allah Amridhie- amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema, *"Atakayejitakasa (kutawadha) nyumbani kwake, kisha akaelekea katika nyumba ya Allah, ili kutimiza moja ya faradhi za Allah, hatua zake hufuta dhambi, na nyingine huinua daraja lake."* [Imepokewa na Muslim: 1521].

* Na pia amepokea ya kwamba Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - alisema: *"Je, nisiwaambieni yale ambayo kwayo Allah Hufuta madhambi na Hunyanyua daraja."*

*Wakasema: "Tuambie, Ewe Mtume wa Allah!" Akasema: "Kutawadha wakati wa ugumu, na kuchukua hatua nyingi kwenda Misikitini, na kungojea Swalah baada ya Swalah, hiyo hasa ndiyo Ribat, (kujizuia kuliko bora zaidi)...".* [Imepokewa na Muslim: 251].

***** Na pia inapokewa kutoka kwake (Abuu Hurayra), kutoka kwa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mwenye kwenda msikitini (wakati wa asubuhi) au kwenda msikitini (wakati wa jioni) Allah Amemuandalia makazi peponi, kila anapokwenda msikitini wakati wa asubuhi, au anapokwenda wakati wa jioni".* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 662,1524. Hili ni tamko la Imam Muslim]

** Na haya makazi ni wadhifa na takrima maalum kwake.

# Swala za Sunna kabla na Baada ya Swala za Faradhi:

Kushikamana na kutekeleza Swala za Sunna (kabla na baada ya Swala ya Faradhi) huleta mapenzi ya Allah, na hupata mtu bishara njema ya Mtume ya kujengewa Nyumba peponi.

*Hadithi iliyopokewa na mama Habiba, mke wa Mtume - Allah Amiwie Radhi - ya kuwa amemsikia Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - anasema: *"Hakuna mja Muislam atakaye swali kwa ajili ya Allah kila siku Rakaa kumi na mbili kwa kujitolea, zisizo za lazima, ila Allah atamjengea nyumba peponi, au ila atajengewa nyumba peponi."* [imepokewa na Muslim 1696].
Na swala hizo za Sunna ni: Rakaa mbili kabla ya Al-Fajiri, Rakaa nne kabla ya Adhuhuri, Rakaa mbili baada ya Adhuhuri, Rakaa mbili baada ya Maghribi, na Rakaa mbili baada ya Al-Ishaa.

## Dua baina ya Adhana na Iqaama

Kutoka kwa Anas bin Malik - Allah Amridhie - amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - Amesema: *"Dua (kujibiwa) iliyo baina ya Adhana (wito wa Swala) na iqaamah haikataliwi."*[Imepokewa na Abu Daawuud na Al-Tirmidhiy 437, 212].

Kusubiri Swala

**a) Kunafanana na ubora wa Swala:**

Kutoka kwa Abu Huraira – Allah Amridhie- kwamba Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Hatoacha kuwa mmoja wenu (anahisabika) yupo kwenye Swala maadamu Swala ndio inayo mzuia."* [Wameipokea Bukhari na Muslim: 659, 649].

**b) Kuombewa msamaha na Malaika:**

Hatoacha kuwa mja anazingatiwa yupo kwenye Swala, muda ambapo atakuwa kwenye mswala wake anangojea Swala, na wanasema Malaika: *"Ee Allah, msamehe, Ee Allah mrehemu, mpaka aondoke au atengukiwe na Udhu."* [Imepokewa na Imam Muslim: 649]

**c) Kufutwa makosa na kupandishwa daraja:** Kutoka kwa Abu Hurairah - Allah Amridhie - kwamba Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - alisema: *"Je, nisiwaambieni yale ambayo kwayo Allah Hufuta madhambi na Hunyanyua daraja?"* Wakasema: 'Tuambie Ewe Mtume wa Allah!' Akasema: *"Kutawadha wakati wa ugumu, na kuchukua hatua nyingi kwenda Misikitini, na kungojea Swalah baada ya Swalah, hiyo ndiyo Ribaat (kujizuia kuliko bora zaidi)...."* [Imepokewa na Muslim: 251].

# Kujishusghulisha na Dhikri na Kusoma Qur'an.

Na miongoni mwa mambo anayopaswa kuyafanya Muislamu anaposubiri Swala ni kujishughulisha na Dhikri (Uradi) na usomaji wa Qur'an. Kwa sababu hayo yana malipo makubwa, na miongoni yaliyopokewa kuhusu hayo ni:

**a) Ubora wa kusoma Qur'ani Tukufu:**
Imepokewa na swahaba Abdallah Ibn Masoud – Allah Amridhie - amesema: Mtume amesema – Rehema na Amani zimshukie:- *"Mwenye kusoma herufi moja katika Kitabu cha Allah anapata jema kwa kusoma kwake, na jema hulipwa mara kumi mfano wake, Sisemi Alif, Laam, Miim, ni herufi moja, lakini Alif ni herufi, Laam ni herufi, na Miim ni herufi."* [Imepokelewa na Al-Tirmidhiy 2910].

* Kutoka kwa Abu Umaamah Al-Bahiliy – Allah Amridhie - amesema: Nimemsikia Mtume – Rehema na Amani ya Allah ziwe juu yake - akisema: *"Someni Qur'an! Kwani itakuja Siku ya Qiyaama kuwa ni muombezi kwa watu wake (wenye kuisoma)."* [Imepokewa na Muslim: 804].

## b) Kusoma *Surat Al-Ikhlas* ni sawa na kusoma Theluthi moja ya Qur-ani Tukufu:

Kutoka kwa Abuu Said Al-Khudriy – Allah Amridhie - amesema: Nabii - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Hivi mmoja wenu anashindwa kusoma theluthi ya Qur'ani katika usiku mmoja?"* Basi likawa zito jambo hilo kwao, wakasema: "Ni nani miongoni mwetu awezaye hayo, Ewe Mtume wa Allah?' *Akasema: "Qul-Huwa Llahu, ni sawa na Theluthi ya Qur'ani."* [Bukhari na Muslim: 5015, 811].

## c) Ubora wa kusoma sura mbili za kinga (*Surat Al-Naas* na *Al-Falaq*)

Kutoka kwa Uqbah bin Aamer - Allah Amridhie - amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake – amesema, *"Hivi, hukuziona Aya zilizoteremshwa usiku wa leo, ambazo hazijaonekana mfano wake? "Sema, najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko." na "Sema, najikinga kwa Mola wa watu."* [Imepokewa na Muslim: 814]

## d) Kusoma *Sura Al-Mulk* inamuombea msomaji wake mpaka asamehewe.

Kutoka kwa Abu Hurairah - Allah Amridhie - kutoka kwa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Sura miongoni mwa sura za Qur'ani, ina Aya Thelathini na tatu, iliyomuombea mtu mpaka akasamehewa, nayo ni Sura ya Tabaaraka Alladhiy Biyadihi Al-Mulk".* [Imepokewa na Al-Tirmidhiy 2891]

# Kuleta Dhikri (Uradi)

**1) Fadhila ya kuleta Tasbihi** (سبحان الله وبحمده)**:**
Imepokewa kutoka kwa Abu Hurayrah - Allah Amridhie - kwamba Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mwenye kusema: Ametakasika Allah, na Sifa Njema ni Zake kwa siku moja mara mia* (سبحان الله وبحمده)*, atasamehewa madhambi yake hata yakiwa kama povu la bahari."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 6405, 2691]

*Na kutoka kwa Mus'ab bin Saad amesema: Baba yangu aliniambia, akasema: Tulikuwa pamoja na Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - Akasema. *''Je, mmoja wenu hawezi kupata mema Elfu moja kila siku?"* Muulizaji akamuuliza katika watu alio kaa nao: "Vipi ataweza mtu kupata mema Elfu moja kila siku?" Akasema: *"Amtakase Allah* ( سبحان الله) *mara mia moja, na huandikiwa mema elfu moja, au huondolewa madhambi elfu moja."* [Imepokewa na Muslim:89].
*Kutoka kwa Abu Hurayrah - Allah Amridhie - amesema: Mtume wa Allah: -Rehema na Amani

za Allah ziwe juu yake – amesema, *"Hakika kusema: Ametakasika Allah, Sifa Njema zote ni za Allah, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, na Allah Ndiye Mkubwa zaidi, hilo lapendeza zaidi Kwangu kuliko chochote kilicho chomozewa na jua."* [Muslim: 2695].

*Na pia inapokewa kutoka kwake (Abuu Hurayra) amesema: kasema Mtume wa Allah – Rehema na Amani nza Allah ziwe juu yake-: *"Mwenye kusema asubuhi na jioni: Ametakasika Allah, na Sifa Njema ni Zake mara mia, hakuna atakaye kuja Siku ya Kiyama, na kilicho bora kuliko kile alichokileta yeye, isipokuwa mtu aliyesema sawa na alivyosema, au akaongeza zaidi yake."* [Imepokewa na Muslim: 2692]

* Pia imepokewa kutoka kwake: - Allah Amridhie - kutoka kwa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Maneno mawili ambayo ni mepesi katika Ulimi, mazito kwenye Mizani, yana pendeza sana kwa Mwingi wa Rehema: Ametakasika Allah na kila upungufu, na Sifa Njema ni Zake, Ametakasika Allah na kila upungufu, Aliye Mtukufu."*

[Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 6406, 2694] Na haya matamshi ni ya Imam Muslim.

* Kutoka kwa Samura bin Jun-dub – Allah Amridhie - amesema: kasema Mtume wa Allah: - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - *"Maneno yanayopendwa zaidi na Allah ni manne: Ametakasika Allah, Sifa Njema ni za Allah, Hapana mola ila Allah, na Allah Ndiye Mkubwa, haikudhuru kwa lolote utaloanza nalo."* [Imepokewa na Muslim: 2137).

## 2. Fadhila za neno Hapana mola wa kuabudiwa kwa haki ila Allah, hana mshirika, Ufalme ni Miliki Yake, Sifa Njema ni Zake, na Yeye ni Muweza wa kila kitu:

Imepokewa na Abu Hurairah -Allah Amridhie- kwamba Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mwenye kusema: hapana Apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah Pekee, Hana mshirika, Ufalme ni Miliki Yake, Sifa Njema ni Zake, na Yeye ni Muweza wa kila kitu, mara mia moja kwa siku, atapata*

*malipo ya sawa na aliyewaacha huru watumwa kumi, na huandikiwa mema mia moja, na hufutiwa maovu mia moja. Na itakuwa ni kinga yake dhidi ya Shetani kwa siku ile mpaka jioni, na hakuja mtu na jambo bora zaidi ya alichokuja nacho, isipokuwa atakayefanya zaidi yake."* [Imepokewa na Al-Bukhari na Muslim: 3293, 2691]

## 3. Fadhila za kusema: Hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kutoka kwa Allah:

Kutoka kwa Abu Musa Al-Ash-ary - Allah Amridhie - Amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - aliniambia: *"Ewe Abdallah bin Qais!"* Nikasema: *'Labbayka Ewe Mtume wa Allah' Akasema: 'Je, Nisikuongoze kwenye khazina za Peponi?"* Nikasema: "Niambie, Ewe Mtume wa Allah, - Baba yangu na mama yangu watolewe (kafara kwa ajili yako)." Akasema: *"Hakuna hila wala nguvu ila kwa Allah."* [Imepokelewa na Bukhari na Muslim:4205,2704].

# Kunyosha Safu

## Miongoni mwa Faida na Fadhila Zake, ni Zifuatazo:

### a) Kuitikia amri ya Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake.

Kutoka kwa Abuu Musa - Allah Amridhie - amesema: Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake – amesema, *"Mnaposwali, simamisheni (Nyosheni) safu zenu."* [Imepokewa na Muslim: 404]

### b) Kuafikiana mioyo na madhumuni:

Kutoka kwa Al-Nuuman bin Bashir - Allah Amridhie - amesema: amesema Nabii - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake – amesema, *"Mnyooshe safu zenu, au Allah afarikishe baina ya nyuso zenu."* [Al-Bukhari na Muslim:717, 436]

## c) Inachukuliwa kuwa ni katika kusimamisha Swala:

Kutoka kwa Anas bin Malik –Allah Amridhie - kutoka kwa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Nyoosheni safu zenu, kwani kunyosha safu ni katika kusimamisha Swala."* [Imepokewa na Al-Bukhari na Muslim: 723, 433].

## d) Ina vikwazo kwa Mashetani:

Kutoka kwa Abdullah ibn 'Umar - Allah Amridhie - kwamba Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Simamisheni (Nyoosheni) safu, na wekeni sawa mabega yenu, zibeni mianya. Na kuweni wapole kwa ndugu zenu, na wala msimwachie Shetani nafasi ya wazi."* [Imepokewa na Abu Daud: 666].

## e) Yeyote anayeunganisha safu, Allah Atamunganisha:

Kutoka kwa Abdullah bin 'Umar - Allah Amridhie - amesema: Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"... na atakayeunganisha safu, Allah Atamunganisha, na mwenye kuikata basi Allah Atamkata."* [Imepokewa na Dawood: 666].

# Fadhila za Kuswali

## a) Kupata cheo, na msamaha wa dhambi, na Riziki iliyo bora:

Allah Mtukufu Amesema: *"Wale wanaoisimamisha Swalah na katika Tuliyowapa basi hutoa * Hao ndio Waumini ambao ni wa kweli, wana vyeo, na msamaha na riziki bora kutoka kwa mola wao mlezi".* [Al-anfaal: 3-4]

Na Allah Akasema - Utukufu ni Wake - *"Na uwaamrishe watu wako kuswali, na uendelee mwenyewe kwa hayo, sisi hatukuombi riziki, bali sisi ndio Tunakuruzuku, na mwisho mwema ni kwa mcha mungu."* [Twaha: 132]

## b) Kufutiwa madhambi na makosa:

Allah Mtukufu Amesema: *"Na simamisha Sala katika ncha mbili za mchana na mwanzo wa usiku, hakika matendo mema huondoa maovu, huo ni ukumbusho kwa wanao kumbuka."* [Huud: 114.].

* Abu Hurairah - Allah Amridhie - amesema: Alimsikia Mtume wa Allah - Rehema na Amani ziwe juu yake - akisema: *"Mwaonaje lau kama*

*mto ungekuwa upo kwenye mlango wa mmoja wenu, akawa anaoga humo kila siku mara tano, je utabaki uchafu kwake wowote?"* Wakasema: "Hautabaki uchafu wowote.*" Akasema: "Hayo ni kama Swala tano za kila siku, ambazo kwazo Allah Hufuta dhambi."* [Bukhari na Muslim: 528, 667]

* Na amepokea pia Abu Hurairah - Allah Amridhie - amesema: Alikuwa Mtume wa Allah akisema: *"Swala tano za kila siku, na Ijumaa hadi Ijumaa, na Ramadhani hadi Ramadhani ni kafara ya yaliyotokea (katika madhambi) kati kati yake, yakiepukwa Madhambi makubwa."*[Imepokewa na Muslim: 233].

**c) Kukirimiwa kwa Urithi wa Pepo ya Firdausi:**

Allah Mtukufu Amesema: *"Na wale wanao zihifadhi Sala zao * Hao ndio warithi * Ambao watarithishwa pepo ya Firdausi ya juu, wao wataishi humo milele".* [Muuminuna aya: 9-11]

## d) Kupata Rehema:

Allah Mtukufu Amesema: *"Na simamisheni Swala na toeni Zaka na Mtiini Mtume ili mpate kurehemewa."* [Al-Nur: 56]

## e) Swala ni nuru kwa mwenye kuiswali:

Imepokewa na Abu Maliki Al-Ash-ary - Allah Amridhie - amesema: Mtume – Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema *"Swala ni nuru, Sadaka ni dalili (ya Imani), Subira ni mwangaza, na Qur'an ni hoja itakayokusaidia kwako au itakuwa dhidi yako. Kila mtu anatoka mapema, atakuwa mwenye kuiokoa nafsi yake (na Moto) au ataiangamiza."* [Imepokewa na Muslim: 223].

# Ubora wa Swala ya Jamaa

Allah Amesema: *"Katika Nyumba ambazo Allah, Ameamrisha zitukuzwe, na humo litajwe Jina Lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni * Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Allah na kushika Swala, na kutoa Zaka, wanaikhofu siku ambayo nyoyo na macho yatageuka."* [Al-nur: 36,37]

Kutoka kwa Abdullah bin 'Umar - Allah Awaridhie - kwamba Mtume wa Allah –Rehema na Amani zimshukie - amesema: *"Swala ya jamaa ni bora kuliko Swala ya mtu mmoja kwa daraja Ishirini na saba."* [Imepokewa na Al-Bukhari na Muslim: 645, 650]

# Fadhila za Baadhi ya Swala

## Swala za Al-Fajiri na Al-asiri:
## a) Malaika wa usiku na Malaika wa mchana wanashuhudia.

*"Shika Swala Jua linapopinduka mpaka giza la usiku, na Qur'ani ya Alfajiri. Hakika Qur'ani ya Alfajiri inashuhudiwa."* [Al-Isra: 78]

Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amridhie - amesema: Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema, *"Wana badilishana kati yenu Malaika wa usiku na Malaika wa mchana, na wanakusanyika kwa ajili ya Sala ya Al-Fajiri, na Al-Asr (wanasali pamoja). Kisha watapanda miongoni mwao wale waliokuwa usiku nanyi, na Allah Atawauliza - na Yeye Anawajua zaidi – 'Vipi mliwaacha waja wangu?' Watasema: 'Tuliwaacha wakiwa wanaswali, na tukawajia wakiwa wanaswali."* [Al-Bukhari na Muslim: 555, 632

## b) Kuingia Peponi:

Imepokewa kutoka kwa Abuu Musa - Allah Amridhie - kwamba Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mwenye kuswali nyakati mbili zenye baridi (Sala ya Al-fajiri na Al-Asri) ataingia Peponi."*[Ameipokea Bukhari na Muslim: 574-635].

## c) Kutoingia motoni:

Kutoka kwa Umara bin Ruaiba - Allah Amridhie - amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - akisema: *"Hataingia Motoni yeyote anaye swali kabla ya kuchomoza jua, na kabla ya kuzama kwake."* [Imepokewa na Muslim: 634].

## d) Mja kuwa chini ya Hifadhi na Dhima ya Allah:

Kutoka kwa Jun-dub bin Abdallah - Allah Amridhie - amesema: Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mwenye kuswali Swala ya Al-fajiri yuko kwenye Hifadhi ya Allah, basi Allah hawatakii ninyi ulinzi wa chochote."* [Amepokea Muslim 657].

## h) Kumuona Allah:

Kutoka kwa Jariyri - Allah Amridhie - amesema: Tulikuwa tumekaa mbele ya Mtume - Rehema za Allah ziwe juu yake - Akaangalia Mbinguni usiku wa Mwezi kumi na nne, akasema: *"Hakika nyinyi mtamuona Mola wenu Mlezi kama mnavyouona huu mwezi, hamtapata tabu katika kumuona Yeye. Na ikiwa mtaweza kutoshindwa kuswali kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa jua, basi fanyeni hivyo".* [Amepokea Al-Bukhari na Muslim: 7434, 633]

## Fadhila Za Swala Ya Isha Na Al-Fajiri:

Kutoka kwa Uthman - Allah Amridhie - amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - anasema: *"Mwenye kuswali Swala ya Ishaa katika jamaa, ni kama amesimama (kuswali) nusu ya usiku, na anaye swali swala ya Alfajri ni kama vile amesimama usiku wote".* [Amepokea Muslim: 656]

### Fadhila za Unyenyekevu katika Swala:

**a) Kufaulu na kupata Pepo ya juu kabisa:**
Allah Mtukufu Amesema: *"Wamefaulu Waumini* * *walionyenyekea katika Sala zao* * *na wanaojiepusha na maneno ya upuuzi." Mpaka Maneno Yake Allah: "Hao ndio warithi. Watakaorithi Pepo ya juu (AlFirdaus) watakaa humo milele."* [Al-Muuminun: 1-11].

**b) Kuzidi ujira wa Swala:**
Kutoka kwa Ammar Ibn Yasir - Allah Amridhie - amesema: nimemsikia Mjumbe wa Allah - Rehema na Amani zimfikie - anasema: *"Hakika*

*mja huswali Swala ambayo hapati malipo yake isipokuwa moja ya kumi, moja ya tisa yake, moja ya nane yake, moja ya saba yake, moja ya sita yake, moja ya tano yake, robo yake, theluthi yake, nusu yake."* [Imepokewa na Imam Ahmad katika Mus-nad wake: 4/321].

## c) Kusamehewa madhambi na kupata ujira mkubwa:

Allah Amesema: *"Hakika waislam wanaume na waislam wanawake, na waumini wanaume na waumini wanawake, na watiifu wanaume na watiifu wanawake, na wasemao kweli wanaume na wanawake, na wenye subira wanaume na wanawake, na wanyenyekevu wanaume na wanawake, na watoao sadaka wanaume na wanawake, na wanao funga wanaume na wanawake, na wanao hifadhi tupu zao wanaume na wanawake, na wanao mkumbuka Allah kwa wingi wanaume na wanawake, hao Allah Amewaandalia Msamaha na ujira mkubwa."* [Al-ahzab: 35]

## Dua ya Kufungua Swala:

### Hufungua Milango ya Mbinguni:

Kutoka kwa Ibn 'Umar - Allah Awawie radhi - amesema: Tukiwa tunaswali pamoja na Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - pale mmoja katika watu aliposema: "Allah Ndiye Mkuu, na Sifa Njema zote ni za Allah, na Utukufu ni wa Allah, asubuhi na jioni." Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake – akasema, *"Nani aliye sema kadhaa na kadhaa?"* Akasema: "Mimi Ewe Mtume wa Allah!" Akasema: *"Nimeshangazwa nayo, imefunguliwa milango ya mbingu kwa sababu yake."* Ibn Umar - Allah Amridhie – anasema, 'Sikuyaacha hayo maneno tangu nilipomsikia Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - akisema hivyo." [Imepokewa na Muslim: 601].

# Kusoma Surat Al-Fat-Ha

## a) Ndio Sura kubwa zaidi kwenye Qur'an:

Imepokewa na Abii Saidi Bin al-Mualla - Allah Amridhie - amesema: Nilikuwa naswali Msikitini, akaniita mimi Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - nami sikumjibu, kisha nikasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Hakika mimi nilikuwa naswali.' Akasema, *'Hivi hakusema Allah: "Enyi mlio amini! Muitikieni Allah na Mtume anapokuitieni jambo la kukupeni uhai."* kisha akaniambia: *"Nitakufundisha Sura, hiyo ni Sura kubwa kwenye Qur'ani, kabla hujatoka Msikitini"* kisha akanishika mkono wangu, na alipotaka kutoka nikamuambia: 'Hivi hukuniambia kuwa nitakufundisha Sura kubwa katika Qur-an?" Akasema: "الحَمـدُ لله ربِّ العَـالمين" *Hizo ni Aya saba zinazosomwa mara kwa mara, na Qur'ani Tukufu, ambayo nimepewa.*" [Imepokelewa na Bukhari: 4474]

## b) Sifa na Dua:

Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amridhie - amesema: Nimemsikia Mjumbe wa Allah - Rehema na Amani ziwe juu yake - akisema: *"Amesema Allah – Mtukufu - Nimeigawa Swala kati yangu na Mja wangu nusu mbili, na Mja wangu atastahiki (kupata) anachokiomba, akisema Mja 'Al-Hamdulillahi Rabbi Al-'alamiyna' anasema Allah: 'Amenishukuru Mja wangu.' Akisema tena: 'Ar-Rahmani Ar-Rahim' Anasema Allah: 'Amenisifu mja wangu.' Akisema tena: 'Maliki yawmi Ad-Diyni.' Anasema Allah: 'Amenitukuza Mja wangu.' Akisema tena: 'Iyyaaka na-'abudu wa Iyyaaka Nasta'inu' Allah Anasema: 'Hili ni kati Yangu na Mja wangu, naye atastahiki kupata alicho kiomba.' Akisema tena: 'Ihdinaa sswiraatwa Al mustaqiyma, swiraatwa Al-ladhiyna An'amta 'Alay-him ghayril Maghdhuubi 'Alayhim wala Ddhwaa-liyna' Allah Anasema: 'Hili ni la mja wangu, naye atastahiki kupata alicho kiomba."* [imepokelewa na Muslim: 395]

## Msamaha wa Madhambi kwa Kuitikia Dua

* Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amuwie radhi - Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Ataposema Imam*: *(غير المغضوب عليهم ولا الضالين) sio wale Ulio wakasirikia wala waliopotea, basi semeni Aamin, hakika yule ambae kauli yake ikiafikiana na kauli ya Malaika, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia yote."* [Bukhary: 782]

* Kutoka kwake pia, ya kwamba Mtume wa Allah amesema: *"Akisema mmoja wenu Amiin, na wakasema Malaika mbinguni: Amiin, moja katika hizo ikaenda sanjari na nyingine, atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia."* [Bukhary na Muslim: 781, 41]

## Fadhila za Rukuu:

Kutoka kwa Ibn 'Umar - Allah Awaridhie - amesema: nimemsikia Nabii - Rehema na Amani ziwe juu yake - anasema: *"Hakika Mja akisimama kuswali huletwa madhambi yake, yakawekwa kichwani kwake ama mabegani mwake, kila*

*anaporukuu ama kusujudu huanguka (madhambi)."* [Ameipokea Ibn Hibbani: 5/26].

## Dua ya Kutoka Kwenye Rukuu:

Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amridhie – ya kwamba Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Akisema Imam (سـمع الله لمـن حمـده) amemsikia Allah aliyemhimidi, basi semeni: (اللهم ربنا لـك الحمـد) 'Ewe Allah Mlezi wetu, Sifa zote njema ni Zako, hakika yule ambae kauli yake itaafikiana na kauli ya Malaika, atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia"* [Amepokea Bukhary na Muslim: 796, 409]

Na kwenye Riwaya nyingine, semeni ( ربنـا ولـك الحمـد) Ewe Allah Mlezi wetu, na ni Zako Pekee Sifa Njema.

* Kutoka kwa Rifaa Bin Raafii Al-Zuraqiy - Allah Amridhie - amesema: "Siku moja tulikuwa tukiswali nyuma ya Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - Aliponyanyua kichwa chake kutoka katika Rakaa, akasema: ( سمع الله لمـن حمـده) amemsikia Allah yule aliyemhimidi,

akasema mtu mmoja nyuma yake: ( ربنا ولك الحمد حمدا كثيرا طيبا مباركا فيه), ‘Ewe Mola wetu Mlezi, na ni Zako Pekee Sifa Njema zilizo nyingi, mzuri, na zenye baraka ndani yake.” Alipomaliza akasema: “Nani aliyekuwa anaongea?” Akasema: “Mimi.” Akasema Mtume: *"Nimewaona Malaika zaidi ya Thelathini wakiyaharakia maneno hayo, nani atakuwa wa kwanza kuyaandika".* [Ameipokea Bukhary: 799]

# Sijda

## a) Kupata mafanikio, kufuzu kupata pepo

Allah –Mtukufu- Amesema, *"Enyi mlio amini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mfanikiwe."* [Alhaj: 77]

## b) Fadhila za Allah, Radhi Zake na Nuru siku ya Kiyama.

Allah - Mtukufu Amesema: *"Muhammad ni Mtume wa Allah. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama (kurukuu) na kusujudu, wakitafuta fadhila na radhi za*

*Allah. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu…"* [Al-Fat-h: 29]

## c) Hunyanyuliwa Daraja na Hufutiwa Madhambi:

Kutoka kwa Thauban - Allah Amridhie - amesema: kasema Mjumbe wa Allah – Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, *"Jilazimishe kusujudu sana kwa ajili ya Allah, hakika yako hautosujudu sijda yeyote kwa ajili ya Allah isipokuwa Allah Atakunyanyua daraja na Atakufutia madhambi."* [Amepokea Muslim: 488]

## d) Inapatisha kuwa pamoja na Mtume:

Kutoka kwa Rabia Bin Kaabi al-Aslamiy - Allah Amridhie - amesema: Nilikuwa nalala pamoja na Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - Nikamletea Maji yake ya kutawadha pamoja na mahitaji yake, akaniambia: *'Omba!'* Nikasema: 'Ninakuomba kuwa nawe peponi.' Akasema: '*Na kingine Kisichokuwa hicho.'* Nikasema, 'ndio hicho.' Akasema: *"Basi nisaidie ili ulipate hilo kwa kusujudu sana."* [Amepokea Muslim: 489]

**e) Ni sababu ya kuporomoka madhambi:**
Kutoka kwa Ibn 'Umar - Allah Awaridhie - amesema: nimemsikia Nabii - Rehema na Amani ziwe juu yake - anasema: *"Hakika Mja akisimama kuswali huletwa madhambi yake, yakawekwa kichwani kwake, ama mabegani mwake, kila anaporukuu ama kusujudu huanguka (madhambi yake)."* [Ameipokea Ibn Hibbani: 5/26].

**e) Ni sehemu ya kujibiwa dua**
Kutoka kwa Abii Hurayra - Allah Amridhie - amesema: *"Ukaribu zaidi wa mja na Mola wake, ni pale anaposujudu, basi zidisheni kumuomba."* [Imepokewa na Muslim: 482]

*Kutoka kwa Ibn Abasi - Allah Amridhie - amesema: kasema Mjumbe wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake: *"... ama kwenye sijda jitahidini sana kuomba Dua, kwani ndio sehemu mnayostahiki kujibiwa maombi yenu."* [Imepokelewa na Bukhary na Muslim: 806, 182]

**f) Moto hautaunguza viungo vya kusujudia.**

# Tashahudi ya Kwanza

* **Kupata malipo kwa idadi ya waja wa Allah walioko mbinguni na ardhini:**

Kutoka kwa Abdillahi Bin Masoud - Allah Amridhie - amesema: Tulikuwa tukiswali pamoja na Nabii - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - tunasema:

(السلام على الله قبل عباده، السلام على جبريل، السلام على ميكائيل، السلام على فلان وفلان)

"Amani iwe juu ya Allah mbele ya waja Wake, amani iwe juu ya Jibril, amani iwe juu ya Mikaeli, amani iwe juu ya fulani na fulani alipo maliza Nabii - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - akatuelekea kisha akasema: *"Hakika Allah Yeye ni Salaam (amani), basi akikaa mmoja wenu katika Swala na aseme:*

(التحيات لله والصلوات والطيبات، السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته، السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين)

*"Sifa zote Njema ni za Allah, Swala na kheri, Amani iwe juu yako, ewe Mtume, na Rehema na Baraka za Allah. Amani iwe juu yetu na juu*

*ya waja wema wa Allah." Hakika mtu akiyasema hayo watayapata waja wema wote, wa mbinguni na ardhini-*

(أشـهد أن لا إلـه إلا الله، وأشـهد أن محمـدا عبـده ورسـوله"...)

*"Nashuhudia ya kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake."* [Imekubaliwa na Bukhary na Muslim: 6230, 402]

Kumswalia Mtume katika Tashahudi ya Mwisho:

**a) Ni kufuata kwa ajili ya Allah, na kuwaiga Malaika wake:**
Allah - Mtukufu- Anasema: *"Hakika Allah na Malaika wake wanamsalia Nabii, Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu."* [Al-ahzab: 56]

**b) Ziada ya malipo, hadi nyongeza kwa mara kumi:**
Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amridhie - Hakika Mjumbe wa Allah amesema:

*"Atayenisalia mimi mara moja, Allah Atamsalia mara kumi."* [Ameipokea Muslim: 408]

**c) Kuomba dua kabla ya Salaam:**
Kutoka kwa Abdillahi Bin Masoud - Allah Amridhie - ya kwamba Nabii - Rehema na Amani ya Allah ziwe juu yake - amesema: *"Ataposali mmoja wenu na aseme* (التحيات لله....) *Attahiyaatu lillahi....., kisha achague baada ya hapo maombi ayatakayo."* [Imekubaliwa na Bukhari na Muslim: 6230, 402]

## Dhikri na Matendo baada ya Swala

**a) Msamaha wa Madhambi:**
Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amridhie - kutoka kwa Mjumbe wa Allah - Rehema na Amani ya Allah ziwe juu yake - amesema: *"Atakayemtakasa Allah baada ya Sala (*سبحان الله*), mara thelathini na tatu, akamhimidi Allah (*الحمدلله*), mara thelathini na tatu, na akamtukuza Allah (*الله أكبر*) mara thelathini na tatu, hizo zitakuwa tisini na tisa, akasema: kutimiza mia moja:*

(لا إله إلا الله وحده لا شريك له، له الملك، وله الحمد، وهو على كل شيئ قدير)

*Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah Peke Yake, hana mshirika, Ufalme ni Wake, Sifa Njema ni Zake, na ni Muweza wa kila kitu, atasamehewa makosa yake, hata yakiwa mfano wa povu la baharini (kwa wingi)."* [Muslim: 597]

**b) Kuchuma Fadhila, Daraja, Neema na Kuingia Peponi:**

Kutoka kwa Abuu Hurayra - Allah Amridhie - amesema: Walisema: "Ewe Mtume wa Allah! Wamepata Matajiri Daraja za juu na neema za milele." Akawauliza: '*Kivipi?*' Wakajibu: "Wamesali kama tulivyosali, wamepigana Jihadi kama tulivyopigana na wakatoa kutokana na ziada ya mali zao, ilihali sisi hatuna mali." Akasema: *"Hivi nisiwahabarishe jambo ambalo, mtawafikia waliokuwa kabla yenu na mtawapita wanaokuja baada yenu, na hafikii mmoja wenu mfano wa mnachokifanya isipokuwa afanye mfano wenu: Msabihini Allah (*سبحان الله*) baada ya kila sala mara kumi, Mhimidini Allah (*الحمدلله*) mara kumi, na Mtukuzeni Allah (*الله أكبر*) mara kumi."* [Bukhary: 6329]

* Kutoka kwa Abdillahi bin Amri - Allah Awaridhie - kutoka kwa Nabii - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - amesema: *"Mambo mawili hayahifadhi hayo mja Muislam (kuyadumisha) isipokuwa ataingia Peponi, ambayo ni mepesi, na wanaoyafanyia kazi ni wachache: Kumsabihi Allah baada ya kila Sala mara kumi, Kumhimidi mara kumi, Kumtukuza mara kumi, hilo lahisabika mara mia moja na hamsini kwa ulimi, na mara Elfu moja na Mia tano kwenye Mizani, na Amtukuze Allah mara Thelathini na nne atakapo taka kulala, na Kumhimidi mara Thelathini na tatu, Kumsabihi mara Thelathini na tatu. Hilo lahisabika mara mia moja kwa Ulimi, mara Elfu moja kwenye Mizani."* [Imepokelewa na Abuu Daud: 5065, Al-Tirmidhy: 3410, Al-Nasaaii: 1347, na Ibn Maja: 926]

**Na Sifa zote Njema ni Zake Allah Ambaye kwa Neema Zake ndio hutimia mambo mema.**

# Yaliyomo:

Kutawadha.......................................................3
Dhikr (Uradi) Baada ya Kutawadha ...........................5
Mswaki...........................................................5
Kuwahi Mapema Kwenda Kuswali ..............................6
Kuyarejea Maneno ya Adhana..................................7
Kuleta Uradi (Dhikri) baada ya Adhana .......................9
*Kusamehewa Madhambi:........................................9
*Uombezi wa Mtume ..............................................9
Kutembea Kwenda Kuswali...................................... 10
Swala za Sunna Kabla na Baada ya Swala za Faradhi .. 12
Dua baina ya Adhana na Iqaama............................ 13
Kusubiri Swala ................................................... 13
A: Kunafanana na Ubora wa Swala: ......................... 13
B: Kuombewa Msamaha na Malaika: ........................ 13
C: Kufutwa Makosa na Kupandishwa Daraja: ............. 14
Kujishusghulisha na Dhikri na Kusoma Qur'an. ........... 15
A-Ubora wa Kusoma Qur'ani Tukufu:........................ 15
B-Kusoma Surat Al-Ikhlas ni Sawa na Theluthi Moja Ya Qur-Ani Tukufu: .................................................... 16
C: Ubora Wa Kusoma Sura Mbili za Kinga (Surat Al-Naas na Al-Falaq) ...................................................... 16
D: Kusoma Sura Al-Mulk Inamuombea Msomaji Wake Mpaka Asamehewe. ............................................... 17
Kuleta Dhikri (Uradi) ............................................ 18
1: Fadhila ya Kuleta Tasbihi (سبحان الله وبحمده): ...... 18

2.Fadhila za Neno Hapana Mola Apasaye Kuabudiwa Kwa Haki Ila Allah, Hana Mshirika, Ufalme ni Miliki Yake, Sifa Njema Ni Zake, na Yeye Ni Muweza wa Kila Kitu: ........ 20
3:Fadhila za Kusema: Hakuna Uwezo Wala Nguvu Isipokuwa Kutoka kwa Allah: .................................... 21
Kunyosha Safu .................................................. 22
A: Kuitikia Amri ya Mtume. ....................................... 22
B: Kuafikiana Mioyo na Madhumuni: .......................... 22
C: Ni Katika Kusimamisha Swala: .............................. 23
D: Ina Vikwazo kwa Mashetani: ................................ 23
E: Anaye Unganisha Safu, Allah Atamuunganisha: ....... 23
Fadhila za Kuswali ................................................ 24
A: Kupata Cheo, Msamaha wa Dhambi na Riziki .......... 24
B: Kufutiwa Madhambi na Makosa ............................. 24
C: Kukirimiwa kwa Urithi wa Pepo ya Firdausi: ............ 25
D. Kupata Rehema ................................................ 26
E: Swala ni Nuru kwa Mwenye Kuiswali: ..................... 26
Ubora wa Swala ya Jamaa ...................................... 27
Fadhila za Baadhi ya Swala .................................... 28
A: Malaika wa Usiku na Mchana Wanashuhudia. .......... 28
B: Kuingia Peponi .................................................. 29
C: Kutoingia Motoni ................................................ 29
D: Mja Kuwa Chini ya Hifadhi na Dhima ya Allah ......... 29
H: Kumuona Allah ................................................... 30
Fadhila za Swala ya Isha na Al-Fajiri ........................ 31
Fadhila za Unyenyekevu katika Swala ....................... 31
A: Kufaulu na Kupata Pepo ya Juu Kabisa ................... 31
B: Kuzidi Ujira wa Swala ........................................... 31
C: Kusamehewa Madhambi na Kupata Ujira ............... 32
Dua ya Kufungua Swala .......................................... 33

Hufungua Milango ya Mbingu.................................. 33
Kusoma Surat Al-Fat-Ha........................................ 34
A: Ndio Sura Kubwa Zaidi Kwenye Qur’an.................. 34
B: Sifa na Dua.................................................. 35
Msamaha wa Madhambi kwa Kuitikia Dua ................. 36
Fadhila za Rukuu............................................... 36
Dua ya Kutoka Kwenye Rukuu ............................... 37
Sijda ........................................................... 38
A: Kupata Mafanikio, Kufuzu Kupata Pepo: ................. 38
B: Fadhila za Allah, Radhi Zake na Nuru Kiyama.......... 38
C: Hunyanyuliwa Daraja na Hufutiwa Madhambi.......... 39
B: Inapatisha Kuwa Pamoja na Mtume: ...................... 39
E: Ni Sababu ya Kuporomoka Madhambi: ................... 40
F-Ni Sehemu ya Kujibiwa Dua.................................. 40
Tashahudi ya Kwanza ............................................ 41
Kumswalia Mtume Katika Tashahudi ya Mwisho.......... 42
A: Ni Kufuata kwa Ajili ya Allah na Kuwaiga Malaika. .. 42
B: Ziada ya Malipo, Hadi Nyongeza kwa Mara Kumi…42
C: Kuomba Dua Kabla ya Salaam .............................. 43
Dhikri na Matendo Baada ya Swala .......................... 43
A: Msamaha wa Madhambi:...................................... 43
B: Kuchuma Fadhila, Neema na Kuingia Peponi:.......... 44